

JANGA LA UKIMWI

Na: Davis Milenguko

2008

Dodoma

Moderato

mf Si-ku mi - e - zi mi - a - ka ya - pi - ta *mp* ndu - gu tu - na - kwi - sha kwe li *f* ni ma - te - so tu -

me - va - mi - wa na - lo ja - nga la U - KI - MWI *mp* E - we *mf* E - we Mu - ngu Ba - ba tu - sa - i - di - e. **FINE**

ORGAN

2. Nini cha kufanya wote twajua,
Jama tuchukue (kweli) tahadhari,
Uasherati ngono uzembe mitaani,
Tutateketea wote kabisa.

3. Ndugu tega sikio ufahamu,
Na dalili zake (kweli) zitambue,
Homa za mara kwa mara zitatokea,
Pia uzito wako kupungua.

4. Ona wagonjwa wanavyoteseka,
Wataalamu wetu (kweli) wameshindwa,
Kupata tiba ya hili gonjwa UKIMWI,
Ndugu wote tubadili mtazamo.

5. Tuwakumbuke na waathirika,
Tuwapende wote (kweli) tuwatumze,
Hawakupenda wanyanyaswe na UKIMWI,
Ndugu leo kwangu na kesho kwako.

6. Waziri nanyi viongozi wetu,
Mtufundisheni (kweli) tutambue,
Hata tupange maamuzi ya Busara,
Tusubiri ili tunusurike.

7. Dunia yote inasikitika,
Ulimwengu mzima (kweli) unalia,
Vizazi vinaangamia na UKIMWI,
Mungu tuokoe na janga hili.